

# Kukomesha Ukoloni kwa Msaada na Kuimarisha Amani

**Ufupisho**

peace direct

Adeso African Development Solutions

Alliance for Peacebuilding

WCAPS WOMEN OF COLOR ADVANCING PEACE, SECURITY, AND CONFLICT TRANSFORMATION

# Kuhusu ripoti hii

Mnamo Novemba 2020, Peace Direct ikishirikiana na Adeso, Muungano wa Uimarishaji wa Amani na Wanawake wa Rangi Wanaoendeleza Amani na Usalama, waliitisha mashauriano ya siku tatu mtandaoni ili kujadili suala la ubaguzi wa rangi na jinsi ya 'Kukomesha Ukoloni kwa Misaada'. Zaidi ya watu 150 kutoka kwa sekta za maendeleo, misaada ya kibinadamu, na uimarishaji wa amani walishiriki katika mashauriano hayo kwa siku tatu, na tunawashukuru wote ambao walishiriki ufahamu wao, hadithi na uchanganuzi.

# Utangulizi

Kwa kuwa majadiliano kuhusu mienendo isiyo sawa ya mamlaka katika mfumo wa misaada ya kimataifa yameingia katika hali ya kawaida, wanaharakati wa eneo husika wameendelea kupaza sauti zao kuhusu jinsi mamlaka na rasilimali katika mfumo zinabaki kutawaliwa na kuwa kati ya mashirika na mahusiano fulani ambayo kwa kiasi kikubwa hupatikana Eneo la Kaskazini mwa Ulimwengu.

Licha ya ahadi za kushughulikia ukosefu wa haki katika mfumo, hasa uliotangazwa katika Mkutano wa Kibinadamu Ulimwenguni huko Istanbul mnamo 2016, maendeleo madogo yamefanyika katika maeneo mengi muhimu. Hii ni pamoja na ufadhili wa mashirika ya maeneo husika na jinsi ambavyo uamuzi, mamlaka na udhibiti bado unashikiliwa na idadi ndogo ya wafadhili na INGO.

Kufuatia maandamano ya Maisha ya Watu Weusi yana Umuhimu ambayo yalianza nchini Marekani mnamo 2013 na kupata umaarufu ulimwenguni katika majira ya kiangazi ya 2020, wale wanaofanya kazi katika sekta ya misaada wamelazimika kukabiliana na ukweli kwamba kazi zao wenyewe zimeingia katika ubaguzi wa rangi, jambo ambalo halijajadiliwa au kutambuliwa hata kidogo hadi hivi majuzi.

Kukomesha ukoloni kwa maendeleo, misaada ya kibinadamu na uimarishaji wa amani – harakati ya kushughulikia na kuvunja miundo ya ubaguzi wa rangi na ya kibaguzi na kanuni ambazo zimefichwa katika mfumo wa misaada – kunaibuka kama majadiliano ya haraka, muhimu na yaliyochelewa sana ambayo yanaongeza uzito zaidi kwa mwito uliopo wa kubadilisha mfumo. Ikiwa watunga sera, wafadhili, weledi, wasomi na wanaharakati hawataanza kushughulikia ubaguzi wa rangi na kinachomaanishwa na kukomesha ukoloni kwa misaada, mfumo hauwezi kamwe kujibadilisha kwa njia ambazo zinahamisha mamlaka na rasilimali kwa watendaji wa eneo husika.


DONATE
07911 XX

# Matokeo muhimu

- Mazoea mengi na mitazamo ya sasa katika mfumo wa misaada yanafanana na yametokana na enzi ya ukoloni, ambayo mashirika na wafadhili wengi katika Eneo la Kaskazini mwa Ulimwengu bado wanasita kukubali. Mazoea na kanuni nyingine za siku hizi zinaimarisha mienendo na imani za kikoloni kama vile itikadi ya 'Mkombozi mweupe' inayoonekana katika uchangishaji wa fedha na picha za mawasiliano zinazotumiwa na INGO, kwa miundo ya kishirika ya INGO katika Eneo la Kusini mwa Ulimwengu na mitazamo ya baadhi ya wafanyakazi wa misaada ya kimataifa ya Watu Weupe katika Eneo la Kusini mwa Ulimwengu.

- Mitiririko ya misaada kati ya mamlaka za zamani za kikoloni na maeneo yaliyokoloniwa zamani mara nyingi huangazia uhusiano wao wa zamani wa kikoloni, na mamlaka ya kufanya maamuzi yakijikita katika Eneo la Kaskazini mwa Ulimwengu.

- Ubaguzi wa rangi umeingizwa sana katika desturi za kila siku na utendaji wa kazi wa wale walio katika sekta hiyo ambao umeathiri jinsi wafanyakazi wa eneo husika wanazingatia jumuiya zao na jinsi wanavyoshirikiana na INGO.

- Baadhi ya lugha inayotumiwa katika mfumo wa misaada inaimarisha maoni ya kibaguzi na ya ubaguzi wa rangi wa watu wasio Wazungu. Kirai cha 'Kujenga uwezo' kilitajwa kama mfano mmoja ambao unaonyesha kwamba jumuiya husika na mashirika hayana stadi, wakati maneno mengine, kama 'mtaalamu wa taaluma' yanaendeleza taswira za Eneo la Kusini mwa Ulimwengu kama 'lisilo na ustaarabu.'

- Wataalamu wengi wa sekta ya misaada ya Eneo la Kaskazini mwa Ulimwengu wanajitambua, na sekta pana, kama wanaofanya kazi bila kuegemea upande wowote, ambayo sio tu ubuni, lakini pia inaimarisha mawazo ya 'mkombozi mweupe' na 'macho meupe' ambayo ina mizizi yake katika ukoloni.

- Ubaguzi wa rangi unafaidi mashirika katika Eneo la Kaskazini mwa Ulimwengu na pia wale kutoka Eneo la Kusini mwa Ulimwengu ambao wanajua jinsi ya 'kucheza' na mfumo. Mfano ulioenea zaidi uliotajwa katika mashauriano hayo ulikuwa fursa za ufadhili za mipango na utafiti ambao unafaidi idadi ndogo ya 'watuhumiwa wa kawaida' yaani INGO zilizo na uhusiano wa awali na wafadhili.

- Mojawapo ya dhihirisho dhahiri la ubaguzi wa rangi katika sekta hiyo ni mfumo unaofanana wa kuajiri wafanyakazi katika Eneo la Kusini mwa Ulimwengu, sio tu kwa mishahara na marupurupu yanayotolewa kwa wafanyakazi wa Eneo la Kusini mwa Ulimwengu ikilinganishwa na wenzao wa Eneo la Kaskazini mwa Ulimwengu, lakini pia jinsi stadi na uzoefu hupunguzwa thamani kwa weledi kutoka Eneo la Kusini mwa Ulimwengu.

- Muundo wa mpango na utafiti umejikita katika maadili na mifumo ya maarifa ya Magharibi ikimaanisha kuwa mipango mingi bila kukusudia huunda kiwango kulingana na Magharibi ambayo jumuiya katika Eneo la Kusini mwa Ulimwengu zinatakiwa kutimiza. Ufahamu wa eneo husika, kimsingi, umepunguzwa thamani.

- Changamoto zinazowakabili weledi binafsi wa rangi zinakuzwa ikiwa wao ni wa makundi mengine yaliyotengwa, ikiwemo wanawake, jumuiya ya LGBTQ*, jumuiya ya walemavu, jumuiya ya wasiozungumza Kiingereza, n.k. Majaribio ya kuzuia mgawanyiko wa ulimwengu na eneo husika mara nyingi huzingatia kundi fulani la utambulisho, na hivyo kukosa kuingiza mtazamo wa makutano.

# Jinsi ubaguzi wa rangi unaonekanaje katika tasnia




AID

# Mapendekezo

## Mapendekezo kwa wafadhili, INGO na watunga sera

### Tambua kwamba ubaguzi wa rangi upo

Kukubali kwamba ubaguzi wa rangi upo haufuti uzuri ambao sekta hiyo inafanya, wala haimaanishi kukataa kabisa misaada/ushirikiano wa kimataifa. Aidha, kukiri hakumaanishi hatia ya kibinafsi. Hata hivyo, kuna jukumu la pamoja la kupambana na tatizo hili. Wafadhili na INGO wanaweza kusaidia kwa kukagua mawazo na mazoea yao, katika mchakato wa kukagua jinsi ubaguzi wa rangi unaweza kuonekana katika kazi yao (angalia mchoro X). Hii inaweza kuhusisha kuchunguza jinsi mawazo ya ubaguzi wa rangi, ya kibaguzi au ya upendeleo yameathiri uhusiano wa wafadhili au INGO na mashirika ya eneo husika na watu, hasa ikiwa watendaji wa eneo hilo wana vitambulisho vingi vilivyotengwa. Hatua muhimu ya kwanza itakuwa kuweka taarifa kwa umma kwenye tovuti ya shirika na katika vifaa vyake vya mawasiliano ikikiri mamlaka na msimamo wake ndani ya mfumo wa misaada, upendeleo ambao unaweza kuwa umefahamisha hatua za zamani za shirika hilo, na mamlaka ya kimfumo ambayo huwapendelea watu fulani zaidi ya wengine.

### Himiza mazungumzo na wafadhiliwa na jumuiya kuhusu mamlaka

Wafadhili, watunga sera na INGO wanahitaji kutumia muda mwingi kusikiliza wasiwasi wa makundi ya eneo husika na jumuiya kuhusu kutokuwa na usawa wa mamlaka katika mfumo wanapoendelea na mahitaji yao ya nyenzo, uchumi na stadi. Mazungumzo kuhusu mamlaka, ni nani anayeshikilia na jinsi inavyotekelezwa hayatatoka mara nyingi kwa makundi ya eneo husika. Kwa hivyo, wafadhili na INGO wanahitaji kuruhusu fursa za kukosoa mamlaka na mazoea yao. Hii inaweza kuanza kwa kuwaomba wafadhili kukamilisha utafiti usiowatambulisha ambao unahitaji maoni yao kuhusu shirika, wafanyakazi wake na mwingiliano wao wa zamani. Hii inaweza kukuzwa kwa kukusanya maoni ya kina kutoka kwa wafadhiliwa. Mchakato kama huo unaweza kuunda msingi wa mazungumzo na kuunda mazingira ambayo yataruhusu jambo hili.

### Unda nafasi ya mabadiliko

Mabadiliko yanayohitajika katika mfumo yatasukumwa na wahusika katika wigo mzima, kwa hivyo ni muhimu kwamba wafadhili na INGO waunde nafasi na fursa kwa makundi ya eneo husika, mashirika na wafadhiliwa kushiriki uzoefu na kuweka mikakati pamoja. Ni muhimu sana kuunda nafasi zinazohusisha wale walio na vitambulisho vilivyotengwa zaidi, kama vile wanawake, vijana na walemavu. Wakati mikakati kama hiyo inaweza kusababisha makundi kupinga mamlaka ya shirika au mtu binafsi, lazima wawe tayari kukubali jambo hili, hata isipowafurahisha. Kwa kweli, ikiwa mazungumzo kuhusu mamlaka yanafurahisha, kuna uwezekano mkubwa kwamba maoni wazi au ya kweli hayashirikiwi, au kwamba mazingira yanayofaa ya kuwezeshwa yameundwa. Wafadhili na INGO wanapaswa pia kujua kwamba baadhi ya makundi yatadai nafasi ya mabadiliko, badala ya kungojea kualikwa katika nafasi mpya iliyoundwa, na lazima wawe tayari kuachilia udhibiti wa michakato hii.

### Kuwa makini kwa kile unachosema

Kukagua upya lugha iliyopo, na vile vile kukubali lugha mpya na istilahi, kunaweza kusaidia katika kuhama kutoka kwa mifumo iliyojikita katika historia za wakoloni na mitazamo mipya, jumuishi na ya ubunifu. Wafadhili na INGO wanapaswa kuondoa maneno ambayo hayafai tena, kama vile 'wanufaika', 'kujenga uwezo' na hata 'misaada' (neno linalotumika katika ripoti hii). Jumuiya husika zinapaswa kuruhusiwa kuongoza mabadiliko katika istilahi, na mashirika kuzikubali panapowezekana na kutathmini upya pasipowezekana.

## Kuhimiza desturi wa uwazi wa kukosolewa

Desturi inahitaji kubuniwa ambayo inapingana kabisa na lugha na mazoea ya ubaguzi wa rangi, ya kibaguzi na ya upendeleo. Hii inahitaji kila mtu kuzungumza wanaposhuhudia visa vya ubaguzi wa rangi na/au vya kibaguzi, badala ya kuwapa watendaji wasio Wazungu, wasio Wa Magharibi jukumu hilo. Hii inahitaji mashirika yote kuanzisha nafasi salama za kukosoa kindani, haswa kwa watu wa rangi ndani ya mashirika yanayotawaliwa na Wazungu. Nafasi hizi salama lazima zitambue jinsia, umri na mambo mengine yoyote ambayo yanaweza kuathiri utayari wa mtu kukosoa. Kwa kuongezea, viongozi wa mashirika wanapaswa kutambua mapungufu yao wenyewe kuhamasisha desturi wa kujitafakari na uaminifu.

## Fadhili kwa ujasiri

'Fadhili kwa ujasiri' ni mwaliko kwa wafadhili kuunda njia za ufadhili ambazo zinaweza kupatikana na za kujumuishwa zaidi, na pia kukubali viwango vikubwa vya kutokuwa na uhakika na uwezekano wa kutofaulu. Wakati wafadhili wanakubali uwezekano wa kutofaulu kwa mpango, hii nafungua mlango wa mitazamo ya ufadhili ambayo ni bunifu na nyumbufu, kama vile wafadhili kuchukua jukumu kubwa la kazi ya ukiritimba au kuchukua hatua maalumu za mafanikio. Jitihada na mifano katika eneo hili ni pamoja na mashirika kukusanya fedha ili kupunguza hatari, ufadhili wa moja kwa moja, ufadhili wa KIJAMII, Mradi wa Uhisani wa Uaminifu, kuweka malengo ya utoaji wa fedha usio na vizuizi kwa mashirika ya eneo husika, kufuata mahitaji ya ukaguzi kwa mashirika ya eneo husika, na kurekebisha vigezo vya ustahiki ambavyo vinapendelea INGO za Magharibi.

## Kuajiri kwa njia tofauti

Mashirika lazima yasitishe mazoea ya kutafuta kwanza wafanyakazi wa nchi za nje kwa nafasi yoyote ya kazi iliyo ng'ambo. Badala yake, inapaswa kudhaniwa kuwa nafasi zote zinaweza kuchukuliwa na wafanyakazi wa eneo husika. Kwa mashirika hayo yaliyo katika 'Eneo la Kaskazini mwa Ulimwengu', INGO zinapaswa kuhakikisha zina sera na mikakati ya kuajiri wafanyakazi anuwai. Nyenzo kama vile WCAPS 'Orgs in Solidarity', taarifa ya mshikamano yenye pointi 12 inapaswa kutumika kama msingi wa kazi hiyo.

## Wekeza katika maarifa ya kienyeji

Sehemu ya kukomesha ukoloni katika mfumo wa misaada ni kuchunguza kile kinachozingatiwa kuwa data halali na ni nani anayechukuliwa kuwa na ujuzi wa kutosha kuikusanya. Wafadhili na mashirika wanapaswa kuwekeza katika watafiti wa eneo husika badala ya kufadhili usafiri wa watafiti wa Magharibi, na utafiti uliojikita katika maadili ya kienyeji na kujumuisha mbinu za asili. Wakati wa kubuni mpango, INGOs inapaswa kushirikiana na viongozi wa eneo husika kuchunguza mifano iliyopo, alama za kumbukumbu na nadharia za mabadiliko, na kukubali mpya zilizojikita katika mitazamo ya eneo husika. Mipango lazima itathminiwe kupitia mifumo maalumu ya kitamaduni, iliyoanzishwa na weledi wa eneo husika. Utaalamu unapaswa kubuniwa upya ili kuhitaji ujumuishaji wa mwongozo kutoka kwa, miongoni mwa wengine, wataalamu wa vijana, wataalamu wa watetezi wa wanawake, wataalamu wa wanawake na wataalamu wa imani/dini, na hivyo kuruhusu masuluhisho ya muktadha, utaalamu wa kiufundi na kufanya uamuzi unaoongozwa na wenyeji. Ili kuhakikisha kuwa uhusiano kati ya wafadhili, INGO na jumuiya husika sio wa kuvutia, matokeo ya mpango na/au utafiti lazima yashirikishwe na jumuiya husika, na inapaswa kutimiza mahitaji yake zaidi ya yale ya shirika.

## Mapendekezo ya INGO haswa

### Hakuna tena kuchangisha fedha kwa mtazamo wa Wazungu

INGO zinapaswa kusitisha mazoea ya kutumia picha na lugha ambayo inadunisha wakala na heshima ya jumuiya katika vifaa vyake vya kuchangisha fedha/uuzaji. Kwa kuongezea, wanapaswa kufanya ukaguzi wa mawasiliano yao ya nje na ya ndani ili kutoa alama ya maboresho ya siku zijazo, na kuzingatia njia mbadala na za kushirikiana za kurekodi juhudi katika Eneo la Kusini mwa Ulimwengu.

### Kubali mawazo ya mpito kwa mikakati ya kishirika

INGO zinapaswa kuzingatia kukubali mawazo ya mpito, kuweka hatua dhahiri zilizo muhimu za uhamishaji wa mamlaka na rasilimali kwa mashirika ya eneo husika. Uangalifu maalumu inapaswa kukaziwa ili kuhakikisha kuwa mashirika ya eneo husika ambayo yako karibu zaidi na Eneo la Kaskazini mwa Ulimwengu na yanayojulikana zaidi na mfumo wa misaada ya kimataifa hayapendelewi. Mawazo kama hayo ya mpito yanapaswa kuwekwa katika mikakati dhahiri ya kishirika ambayo hupima mafanikio kulingana na kiwango ambacho INGO inapunguza, badala ya kupanua athari ya kitamaduni ya shirika (kwa mfano, idadi ya wafanyakazi wanaoajiriwa, kiwango cha mapato yanayovutiwa na idadi ya watu na jumuiya wanaotumikiwa moja kwa moja). Utekelezaji wa moja kwa moja unapaswa kuondolewa ili kuunga mkono kuhamisha rasilimali kwa mashirika ya eneo husika na kuhifadhiwa tu kwa hali za kipekee kwa ombi la mashirika ya eneo husika. Ofisi za nchi zinapaswa kuwa na malengo dhahiri ya kusaidia asasi za asilia za kijamii, ikiwemo kupitisha angalau asilimia 25 ya ufadhili kwa mashirika ya eneo husika, na malengo makubwa zaidi yaliyowekwa kwa miaka 5-10 ijayo.

### Epuka kuzungusha ujanibishaji

INGO zinapaswa kuepukana na 'kuzungusha' (yaani kutafsiri tena au kubuni upya) ujanibishaji ili kutetea msimamo fulani wa kishirika au kuhalalisha hali ilivyo. Mifano ya zoezi hili ni pamoja na kufafanua ofisi ya nchini ya INGO kama 'ya eneo husika' kulingana na idadi ya wafanyakazi walioajiriwa wa nchi hiyo, usajili wa shirika kama shirika la 'Kitaifa' na asilimia ya fedha ambazo inachangisha kitaifa, badala ya kutoka kwa 'mzazi' wake wa kimataifa. Ikiwa INGO ina ofisi ya nchi, inapaswa kukubali utambulisho huu kama INGO na ieleze kupitia mawasiliano ya nje kwamba inajua mamlaka yaliyo nayo na jukumu linalobeba la kuacha madaraka

### Tathmini upya ushirikiano na mashirika ya eneo husika

INGO zinapaswa kusitisha mazoea ya kutafuta 'washirika watekelezaji' wa muda mfupi na badala yake zianzishe ushirikiano wa kimkakati wa muda mrefu ambao haujatambuliwa na mizunguko ya mradi. Kanuni tisa za ushirikiano wa Peace Direct za ushirikiano mzuri zinaweza kuwa mahali pazuri pa INGO kuanza. Hizi ni (1) Kukubali na kupinga kutokuwa na usawa kwa mamlaka; (2) Kukabiliana na ubaguzi wa rangi na upendeleo; (3) Kusaidia na kuwekeza katika uongozi wa eneo husika; (4) Kujitahidi katika uwajibikaji wa pande zote na mafunzo; (5) Anzisha ushirikiano wa muda mrefu; (5) Kutoa ufadhili bila vizuizi; (6) Kubadilika, na kukuza kubadilika na uthabiti na wenzi wako; (7) Kuzingatia rasilimali zisizo za kifedha kama sehemu ya ushirikiano wowote; na (9) Hakikisha kuwa mabadiliko ya ushirikiano ni shughuli ya kushirikiana.

## Mapendekezo kwa ajili ya watu binafsi

### Tafakari utambulisho wako

Ili kuondoa 'mtazamo wa Wazungu' ulioenea ambayo bado unatawala sekta za misaada, maendeleo na uimarishaji wa amani, kila mtaalamu – wale ambao ni wenyeji na wale wanaofanya kazi nje za nchi – lazima watafakari kuhusu motisha yao ya kuhusika katika tasnia hii. Maswali ya kuulizwa ni pamoja na: Utambulisho wako unakupa upendeleo gani? Je, umeimarishaje 'mtazamo wa Wazungu' wa sekta?

### Endelea kuwa mnyenyekevu


Historia ya tasnia ya misaada imejengwa juu ya wazo kwamba Magharibi inashikilia jibu. Kusambaratisha uongozi uliowekwa kunahitaji weledi wa kimataifa wafanye kazi zao kwa unyenyekevu zaidi. Ni muhimu kwamba wabaki kuwa na uwazi wa kukosolewa na kupata maoni kutoka kwa watendaji katika Eneo la Kusini mwa Ulimwengu, na kwamba watafakari maoni hayo. Sehemu ya kuondoa upendeleo kwa maarifa ya Magharibi ni kuwa na uwazi kwa njia za eneo husika za maarifa na uelewa maalumu wa miktadha ya maendeleo, misaada ya kibinadamu na uimarishaji wa amani.

### Ufikiaji wa zamu na mamlaka

Wakati wote wa mashauriano, washiriki walishiriki uzoefu kadhaa wa Mzungu kutoka Eneo la Kaskazini mwa Ulimwengu kupewa ufikiaji na fursa za upendeleo juu ya mtu wa rangi kutoka Eneo la Kusini mwa Ulimwengu. Watendaji wa Eneo la Kaskazini mwa Ulimwengu wanaweza kusaidia kuhamisha mamlaka kuelekea jumuiya ambazo hazikujumuishwa kwa kuelekeza fursa kwa weledi waliotengwa ambao wangepuuzwa. Wale walio na mamlaka ya kitaasisi na nafasi za uongozi wanaweza kuhimiza uwazi katika mazungumzo kuhusu ubaguzi wa rangi, upendeleo na ukoloni. Jukumu linalotekelezwa na weledi kutoka Eneo la Kaskazini mwa Ulimwengu katika kukomesha ukoloni kwa nyanja hizi wakati mwingine litakuwa kutumia mamlaka yao kushinikiza kujumuishwa na wakati mwingine kurudi nyuma, ili kutoa nafasi kwa weledi wa eneo husika kuchukua nafasi hiyo.

### Panga

Wanaharakati wa eneo husika na weledi wanaotaka kupinga ubaguzi wa rangi na kuhamisha mamlaka katika mfumo mara nyingi watajikuta wakiondolewa kwenye majadiliano na wale walio kwenye mfumo ambao wanataka kubaki mamlakani, au hata kudhihakiwa nao. Ili kushughulikia jambo hili, ni muhimu wanaharakati wajipange na kuungana na makundi mengine ya kitaifa na kimataifa. Kuna mitandao na makundi yanayounga mkono ajenda hii, kama mtandao wa NEAR, CIVICUS na mtandao wa START, na vilevile makundi yasiyo rasmi ya wanaharakati walio tayari kuibua suala hili katika kiwango cha kitaifa na kimataifa.




peace direct

Adeso
African Development Solutions

Alliance for Peacebuilding

WCAPS | WOMEN OF COLOR ADVANCING PEACE, SECURITY, AND CONFLICT TRANSFORMATION